maendeleo ya kiuchumi hasa katika kuwajengea vijana uwe-

zinazohusika na utekelezaji wa mradi huu kutoa ushiriki-

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la T-MARC Tanzania, Charles Singili, alisema mradi

pamoja na elimu ya ufundi stadi, afya, uraia, ujasiriamali na uongozi.

katika baadhi ya maeneo kutokana na kuwa na mvua chache".

NIPASHE UK 15.

# Wananchi mikoa saba kunufaika na mradi ufugaji kuku

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MRADI wa kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki (BEVAC) umepanga kuwafikia wananchi 10,000 katika mikoa saba.

Lengo la mradi huo ni kuongeza kiwango cha uzalishaji asali na Tanzania ifikie asilimia 20 ya uuzaji wa bidhaa hiyo katika soko la nje.

Meneja wa mradi huo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ubeligiji, Martin Mgallah, akizungumza na Nipashe jana, alisema tangu mradi huo umeanza mwaka 2021 umeshawafikia wafugaji nyuki zaidi ya 3,000.

Alisema mahitaji ya asali ya Tanzania katika soko la nje ni makubwa lakini kiwango kinachosambazwa ni asilimia nne tu ambacho kimekuwa kikiuzwa katika nchi za Ulaya, Marekani na Urabuni na hivi sasa limepatikana soko jipya la asali nchi Poland.

Mgallah alisema siyo kwamba Tanzania haina uwezo wa kuzalisha asali ya kutosha bali tatizo asali nyingi inapotea kwa sababu ya kukosa ubora.

"Masoko ya nje yana viwango vinavyotakiwa hivyo kinachofanywa na BEVAC ni kuwafundisha wafugaji nyuki ili asali nyingi isipotee iweze kuingia kwenye soko kubwa ambalo lina tija na litaweza kuingizia nchi fedha za kigeni," alisema.

Mgallah alisema mradi huu ambao ni wa miaka minne ulianzishwa kutokana na serikali kuona sekta ya nyuki haina msukumo mkubwa wakati asali ina soko kubwa nje lakini asali ya Tanzania ilikuwa inakosa ubora kwasababu wafugaji walikuwa wakifuga nyuki kwa njia za kienyeji.

"Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuzalisha asali ya kwanza ni Ethiopia na asali ya Tanzania iliyobora inatoka katika misitu ambayo ni asili hivyo masoko ya Ulaya yanapenda sana asali ya Tanzania. Kuanzishwa kwa mradi wa BEVAC ilikuwa ndio suluhisho la kutatua changamoto ya asali," alisema.

Mgallah alisema BEVAC imekuwa ikiwaunganisha wazalishaji wa asali wa mikoa ya Singida, Kigoma, Shinyanga, Katavi, Tabora, Pemba Kusini na Pemba Kaskazini ambako mradi huo unatekelezwa na masoko ya ndani na nje kwa kuwawezesha ili kuyafikia masoko hayo. Alisema: "Wafugaji wa nyuki walijenga fikra kwamba mizinga ni bidhaa ya kupewa lakini sasa hivi elimu tunayowapa tunataka waachane na kutumia mizinga ya kienyeji ambayo kwanza inasababishwa uharibifu wa mazingira tunataka watumie mizinga ya kisasa ambayo hata uzalishaji wa asali ni mkubwa".

CamScanner

Akinwumi Adesina kabla ya mazungumzo yao katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Sharm El Sheikh nchini Misri, juzi. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

UHURU UK 3.

# Wizara: Wananchi msihofu taarifa za ugonjwa wa kimeta

**NA MWANDISHI WETU**

SERIKALI imesema vifo vya watu wawili vilivyotokea Mei 4, mwaka huu, katika Kijiji cha Msaranga, Kata ya Kisale, Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, havihusiani na ugonjwa wa kimeta.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka kwa Kaimu Mganga Mkuu wa Mifugo Tanzania, Dk. Benezeth Lutege, ilisema wizara hiyo inawatoa hofu wananchi kutokana na taharuki iliyojitokeza wilayani Rombo kuhusiana na vifo hivyo.

Dk. Lutege kupitia taarifa hiyo alisema baada ya majibu ya uchunguzi wa kimaabara yanathibitisha kuwa, vifo hivyo havihusiani na ugonjwa wa kimeta ambao hutokana na kula nyama ya ng'ombe aliyeathirika na ugonjwa huo.

Aidha, alibainisha kuwa wizara hiyo inawasisitiza wananchi wa Kijiji cha Msalanga na Watanzania wote kuendelea kuchukua tahadhari za kiafya ikiwa pamoja na kununua nyama zilizokaguliwa na wataalamu wa mifugo waliosajiliwa na Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) na kutoka kwenye mabucha na maduka ya nyama yaliyothibitishwa na serikali kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (TMB).

**DK. BENEZETH LUTEGE**

Aidha, alibainisha kuwa wizara hiyo inawasisitiza wananchi wa Kijiji cha Msalanga na Watanzania wote kuendelea kuchukua tahadhari za kiafya ikiwa pamoja na kununua nyama zilizokaguliwa na wataalamu wa mifugo waliosajiliwa na Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) na kutoka kwenye mabucha na maduka ya nyama yaliyothibitishwa na serikali kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (TMB).

Pia, alifafanua kuwa, ni vyema wananchi wakajua dalili za ugonjwa wa kimeta ambazo ni kifo cha ghafla kwa mnyama aliyeathirika sehemu zote zilizo wazi ikiwamo kutoa damu ambayo haigandi.

Dalili zingine ni watu ambao hugusana au kula nyama ya mnyama mwenye kimeta, kuonyesha dalili za homa, kupumua kwa shida, kichefuchefu, kutapika na malengelenge katika.

"Dalili hizi hazikuonekana kwa wagonjwa wawili waliofariki dunia katika tukio hilo (Kijiji cha Nsaranga)," alisema huku akibainisha kuwa ni nadra kwa mnyama mwenye kimeta kupatiwa matibabu.

TLS yaunda jopo kuchunguza tukio la wakili

## Kutoka Bungeni

NA FRED MAJALIWA, DODOMA

UHURU UK.5.

# Watanzania 3,154 wanufaika mikopo pembejeo za ufugaji samaki, vizimba

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema katika mwaka 2022/2023, wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendelo ya Kilimo (TADB), imetekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba ya pembejeo za ufugaji samaki ikijumuisha vizimba kwa wanufaika 3,154.

Imeelezwa mikopo hiyo pia hutolewa kwa vifaranga vya samaki na chakula cha samaki kuwezesha ufugaji kwa njia ya vizimba nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema hayo jijini hapa jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Busanda, Bryceson Tumaini aliyeuliza serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wavuvi waliounda vikundi na kuanza ufugaji wa vizimba katika Jimbo la Busanda.

Alisema jumla ya wanufaika 3,154 wameainishwa kunufaika na mradi huo ikijumuishwa vikundi 93, kampuni 10, na watu binafsi 32.

Silinde alisema kwa upande wa Geita DC, vikundi vitatu vinatarajiwa kunufaika na programu hiyo ikiwemo kikundi cha Tumaini chenye wanachama 10 kutoka Jimbo la Busanda.

Alieleza vikundi hivyo vimepewa mikopo ya pembejeo za ufugaji samaki katika vizimba yenye thamani ya sh. milioni 69.4 kwa kila kikundi.

Naibu waziri huyo alisema katika mwaka 2023/2024, serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba ya pembejeo za ufugaji samaki kwa kuwezesha ufugaji katika vizimba 893.

Silinde alitoa wito kwa wafugaji samaki nchini wakiwemo wa Busanda, kuendelea kuchangamkia fursa hiyo kwa kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika wa ufugaji samaki.

SER
kuw
mita
Afya
Tab
Dec
jijini
Kas
itaje
X-R
Upu
seri
kitu
ma
mtu
baj
afy
kut

However, when responding, the ... protect the country's resources.

DAILY NEWS Pg 2.

# 893 fishing tanks to benefit from interest free loans

THE government will in the 2023/24 financial year implement a robust project for provision of interest free loans for aqua fishing subsidy in about 893 fishing tanks, National Assembly heard yesterday.

Deputy Minister for Livestock and Fisheries, David Silinde said in the House yesterday that the government under President Samia Suluhu Hassan was fully committed to helping fishermen in the country.

He was speaking in response to a question posed by Busanda legislator, Bryceson Tumaini (CCM), who had wanted to know the government's strategy to empower fishermen/women who had organised themselves in groups to conduct aqua fishing projects in his constituency.

"I want to ask all fishermen and women to continue grabbing this opportunity for loans by joining groups as well as establishing cooperatives in aqua fishing," he insisted.

According to him, during 2022/23, the ministry in collaboration with the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) had initiated the project for provision of soft and interest free loans in fishing subsidies including those engaging in aqua fishing.

Mr Silinde said that about 3,154 persons have so far qualified for the project including 93 groups, 10 companies and 32 individual persons.

In Geita District Council (DC), he said, three groups are expected to benefit from the project including the Tumaini group which has got ten members from Busanda constituency.

"These groups will be given subsidies for aqua fishing amounting to 69.4m/- per each group," added Mr Silinde.

According to fishing experts, there is a technology called Recirculating Aquaculture System (RAS), which uses tanks of different sizes that can grow up to 1,600 fish in just two months.

In 2017, the investment corporation of the National Service (Suma JKT) conducted research on the technology which has so far paid off.